# UKEKETAJI KWA WANAWAKE

Mwaka 1998 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipitisha sheria iliyofanya ukeketaji kwa wanawake kuwa kosa la jinai. Tangu wakati huo, matukio ya ukeketaji yamepungua kutoka asilimia 18 hadi asilimia 10. Kuna maendeleo makubwa na dhahiri katika kukomesha ukeketaji kwa wanawake Tanzania: Wasichana wengi zaidi wanapitia njia mbadala za unyago na matukio mengi zaidi yanaripotiwa na kushughulikiwa na polisi, ikiwa ni matokeo ya mafunzo ya kuongeza uelewa na mafunzo yaliyofanywa hatua kwa hatua kwa maafisa wanaosimamia sheria kuhusu namna ya kukomesha ukeketaji na unyanyasaji wa kijinsia kwa ujumla.

Mmoja kati ya wanawake kumi nchini Tanzania (wenye umri wa miaka 15-49) wamefanyiwa ukeketaji. Kati yao, asilimia 35 wamekeketwa kabla ya kufikia umri wa mwaka mmoja

Hata hivyo, kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ukeketaji nchini Tanzania, kumeelezwa kama eneo lenye kuleta wasiwasi katika utekelezaji wa mikataba ya haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia. Mila potofu na zenye madhara bado zimeendelea kuwa sehemu ya kawaida ya maisha ya watu katika baadhi ya jamii, na kinacholeta wasiwasi ni kwamba kwa kiasi kikubwa ukeketaji umekuwa ukifanywa kwa watoto chini ya mwaka mmoja.

Mwanamke mmoja kati ya kumi (wenye umri wa miaka 15-49) amekeketwa. Kati ya hao, asilimia 35 wamekeketwa kabla ya umri wa mwaka mmoja.

Kuna tofauti kubwa kimikoa kuhusu takwimu za kuenea kwa matukio ya ukeketaji: Ukeketaji umeenea zaidi katika mikoa ya Manyara, Dodoma na Arusha kwa asilimia 58, asilimia 47 na asilimia 41 . Vilevile, ukeketaji umeenea maradufu katika maeneo ya vijijini (asilimia 13) kuliko maeneo ya mijini (asilimia 5).

Takwimu za mwezi Juni 2018 za Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) zinaonyesha kwamba ongezeko la idadi ya watu linahatarisha maendeleo na juhudi zilizofikiwa mpaka sasa kwa kuwa idadi halisi ya wasichana walio katika hatari ya kukeketwa inaongezeka. Kwa ujumla kupungua kwa vitendo vya ukeketaji kulikoshuhudiwa hakutoshi kuleta uwiano wa ongezeko la idadi ya watu linalotarajiwa.




Hali halisi ya ukeketaji kimkoa[1]

*Utambulisho uliotumika na uwasilishaji wa vitu katika ramani hii, haukusudii kwa hali yeyote ile kuelezea maoni kwa upande wa Umoja wa Mataifa kuhusiana na uhalali wa nchi, wilaya/mkoa, mji au eneo au mamlaka yake, au kuhusiana na ukomo wa mipaka yake.*

## SABABU ZINAZOPELEKEA UKEKETAJI KWA WANAWAKE

Ukeketaji umejikita kwenye kanuni na taratibu za kijamii, imani za kiutamaduni na vichocheo vya kiuchumi. Ukeketaji unaonekana kutumika kama njia ya kudhibiti ashki ya kujamiiana kwa wanawake, na katika jamii nyingi, inachukuliwa kama jambo la muhimu katika shughuli za jando na unyago. Simulizi potofu kuhusu ukeketaji zimekuwa zikirudiwa mara nyingi kiasi cha kusadikiwa kuwa ni kweli.




Kuenea kwa ukeketaji wanawake wenye umri kati ya miaka 15-49




Waliofanyiwa ukeketaji kabla ya mwaka mmoja




Tofauti ya ueneaji wa ukeketaji kimikoa




Tofauti ya mijini na vijijini

[1] Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS-MS) 2015-2016.

## MADHARA YA UKEKETAJI

Ukeketaji unakwamisha utendaji kazi wa asili wa mwili wa mwanamke na una madhara makubwa kwa afya ya wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na afya yao kisaikolojia, kimahusiano na afya ya uzazi.

### Madhara ya muda mfupi:

- Kifo kutokana na kutoka damu nyingi na maumivu makali
- Uharibifu mkubwa wa mfumo wa nje wa viungo vya uzazi na maambukizi

### Madhara ya muda mrefu:

- Maumivu makali ya muda mrefu
- Maambukizi – ikiwemo maambukizi ya mara kwa mara ya njia ya mkojo
- Kupungua kwa raha ya kujamiiana
- Madhara ya kisaikolojia, kama vile msongo wa mawazo utokanao na maumivu
- Kuongezeka kwa hatari za kujifungua kwa njia ya upasuaji
- Kuongezeka kwa vifo vya uzazi
- Kuongezeka kwa hatari za vifo vya watoto wachanga
- Kongezeka kwa hatari ya watoto kuzaliwa kabla ya muda
- Kutoka damu nyingi wakati na baada ya kujifungua
- Watoto kuzaliwa na uzito mdogo (njiti)
- Kuna madhara zaidi kwenye njia ya mkojo kwa wagonjwa wenye fistula ambao walifanyiwa ukeketaji.

## MWITIKIO WA KITAIFA KUHUSU KUTOKOMEZA UKEKETAJI

Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA-VAWC) 2017/2018-2021/2022) umeeleza kwa ufasaha kwamba ukeketaji ni mila inayoathiri wanawake na watoto. Tanzania imedhamiria kukomesha kabisa ukatili wa aina zote dhidi ya wanawake na watoto, ikiwemo ukeketaji, kama sehemu ya utekelezaji wa ajenda ya Maendeleo Endelevu ya 2030.

Mwitikio wa jumla wa sekta mbalimbali ni muhimu katika kukomesha ukeketaji. Watendaji katika sekta ya kisheria lazima wafundishwe kuhakikisha kuwa sheria inayozuia ukeketaji inatekelezwa; jamii isisitiziwe kutumia njia mbadala kwenye sherehe za jando na unyango; programu hizo lazima zizingatie makundi mbalimbali yanayojihusisha na ukeketaji wakiwemo mangariba ambao hupata kipato chao kutokana na shughuli hii na sherehe zinazohusiana na jando na unyago; maeneo salama yanapaswa kuanzishwa kwa ajili ya wasichana waliopo katika hatari; na mipango ya sekta ya afya inapaswa kujumisha mikakati ya kuzuia na kutokomeza ukeketaji.






# TAARIFA ZA MAFANIKIO KUTOKA MAENEO MBALIMBALI

**Kupunguza madhara na kuzuia ukeketaji kupitia mafunzo na uelimishaji wa jamii.**

Umoja wa Ulaya unaiunga mkono *Plan International* katika kazi zao na *Children's Dignity Forum (CDF), New Light Children Center Organization (NELICO),* na jumuiya za wenyeji kupunguza na kukomesha madhara ya ukeketaji katika mikoa ya Mara na Geita. Eliza na wanandoa Jackson na Sabayi, ni baadhi ya waliojikita katika mapambano ya kukomesha ukeketaji mkoani Mara. Eliza alifanyiwa ukeketaji akiwa na miaka 14 na alipofikisha miaka 16 aliolewa kama mke wa tatu kwa mwanaume mwenye miaka 32. Alipata matatizo wakati wa uzazi, na vipigo kutoka kwa mme wake . Eliza alifanikiwa kutoroka na mwanaye na kupata mafunzo ya ujasiriamali katika moja ya vituo vya CDF, ambapo alipata ujuzi uliomuwezesha kujihudumia yeye na mwanaye. Plan International na wabia wake huwawezesha manusura kuvunja mzunguko wa ukeketaji na kuwatetea mabinti zao na ndugu zao ili wasikeketwe.

Baada ya Jackson kufahamu madhara ya ukeketaji, aliamua kumuoa msichana aliyempenda bila kujali kama alikuwa amekeketwa au la. Alimuoa Sabayi akiwa na umri wa miaka 23 na kwa pamoja waliamua kwamba hakuna mtoto wao atakayefanyiwa ukeketaji. Mara nyingi wanaume, hususani vijana wa kiume na wavulana, wanapoelewa madhara ya ukeketaji, mara nyingi huwa mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko na kuunga mkono kukomeshwa kwa ukeketaji. Plan International, CDF na NELICO hutumia majukwaa tofauti, ikiwa ni pamoja na klabu za soka, kuwajulisha na kuwapa uwezo wavulana na wasichana kupambana na ukeketaji.

**Njia mbadala katika kutekeleza shughuli za unyago kama sehemu ya programu pana ya kukomesha ukeketaji**

Kituo cha Masanga, pamoja na mtandao wa Kukomesha Ukeketaji (TFGM) unaoundwa na mamia ya watu wanaojitolea katika Wilaya ya Tarime, hutoa mafunzo ya mwezi mmoja kuhusu haki za binadamu, afya ya uzazi na utamaduni wa jamii ya kabila la Wakurya, pamoja na kutoa mafunzo ya ziada mashuleni. Mafunzo hayo hufuatiwa na sherehe ya mahafali. Mchakato mzima ni sehemu ya sherehe ya unyago ambayo huwa ni mbadala wa ukeketaji kwa wasichana katika jamii. Tangu mwaka 2007, zaidi ya wasichana 2,000 wamehudhuria kwenye kambi hiyo. Mafunzo yanalenga kuwalinda wasichana hao kutokana na ukeketaji, ndoa za utotoni na mimba za utotoni, na kuwafanya wabaki shuleni.

UNFPA hutoa msaada wa kuongeza idadi ya wasichana wanaoweza kushiriki kwenye programu hii, na kuhakikisha upatikanaji wa msaada wa kisaikolojia kwa wasichana na wazazi wao. Hii ni sehemu ya programu pana inayoungwa mkono na UNFPA, ambayo inahusisha kujenga uwezo wa vyombo vya habari, polisi, mahakama, walimu na waganga wa jadi katika kuzuia ukeketaji na mwitikio wake.